

MKUU WA MKOA WA MWANZA MHANDISI ROBERT GABRIEL AZINDUA CHANJO YA MATONE YA POLIO KIMKOA WILAYA YA UKEREWE, HALMASHAURI YA WILAYA HIYO IMEWEKA MALENGO YA KUTOA CHANJO LAKI MOJA ELFU NANE MIA TISA THELATHINI NA SABA (WATOTO 108,937) KATIKA TARAFU NNE (04) ZA WILAYA YA UKEREWE.

Mei 18,2022



Akisoma taarifa fupi kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza katika uzinduzi wa chanjo ya matone ya Polio katika eneo la kituo cha Afya Nakatunguru wilayani hapo, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe Dr. Getera Nyangi amefafanua kuwa, Ugonjwa wa Polio umekuwa tishio kwa miaka mingi katika nchi nyingi duniani ikiwemo nchi ya Tanzania, kwa mara ya mwisho Tanzania ilipata mgonjwa wa Polio mwezi Juni 1996, Hivi karibuni nchi ya Malawi ilitoa taarifa ya kuwepo kwa mgonjwa wa Polio mnamo tarehe 17 Feb, 2022, Mgonjwa huyu alipatikana katika mji Mkuu wa Malawi-Lilongwe.

Hata hivyo, kutokana na mwingiliano wa wananchi baina ya Tanzania na Malawi, na tathmini iliyofanywa na Wizara ya Afya na Shirika la Afya na Shirika la Afya Duniani (WHO) nchi yetu ilionekana ni miongoni mwa nchi zilizo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya ugonjwa wa Polio endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa

Dr. Getera ameendelea kueleza kuwa, Wilaya ya Ukerewe ni moja kati Halmashauri 8 za Mkoa wa Mwanza ambapo ina jumla ya wakazi 518,114 kati yao watoto wenye umri chini ya miaka mitano ni 108,937 ambao ndio lengo letu la chanjo yam atone ya miaka mitano

ni 108,937 ambao ndio lengo letu la chanjo ya matone ya Polio. Wilaya ina vituo 38 ambavyo vinatoa huduma ya chanjo pamoja na huduma zingine, na ina vijiji 77 vyenye vitongoji 518 na kaya 81,230 ambazo zinatarajiwa kufikiwa zikiwa na walengwa.

“Tuna vituo vidogo 223 vya chanjo ili kuwawezesha wananchi wanaosafiri kupata huduma hii ya chanjo ya Polio kwa watoto, Vituo hvi vidogo vipo maeneo ya mialo, magulio, stand ya mabasi, kanisani pamoja na shule za watoto wadogo tukiwa na lengo la kuwafikia watoto wengi zaidi watakaopata chanjo ya matone ya Polio katika maeneo na taasisi zetu” amesema Dr. Getera Nyangi.



“Hata hivyo, Halmashauri ya Ukerewe tumepokea dozi 122,000 za Chanjo ya Polio pamoja na vifaa vinavyohusiana na zoezi la uchanjaji vimekwisha pokelewa na kusambazwa katika vituo vyote 38 vya kutolea huduma kuna timu za uchanjaji zinazohusisha watu watatu kwa kila kituo. Wakiwemo wachanjaji 223, watakwimu 223 pamoja na wahamasishaji 223 jumla 669 ambao kwa pamoja watashirikiana kupita nyumba kwa nyumba wakitoa huduma ya chanjo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi” Amesema Dr. Getera Nyangi.

Aidha, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe Dr. Getera Nyangi amefafanua kuwa Ili kufanikisha azma hii, wilaya tayari imetoa mafunzo kwa watoa huduma 669 wa chanjo yam atone ya Polio wakiwemo wachanjaji, watakwimu pamoja na wahamasishaji na wadau mbalimbali wa shughuli za Afya ikiwemo Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwa ajili ya uhamasishaji na kuendelea na zoezi la kuchanja.

Mara baada ya kusomwa taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhandisi Robert Gabriel amesema, Mkoa wa Mwanza umelenga kutoa Chanjo kwa watoto 846,733 na

imejipanga katika vituo 355 ambapo jumla ya watoa huduma 6,909 wamepata mafunzo kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

"Ukerewe ina jumla ya wakazi 518,114 kati yao watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 ni 108,937 ambao ndiyo lengo la chanjo ya Matone ya Polio," amesema Mhandisi Robert Gabriel.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Dkt. Thomas Rutachunzibwa amesema, tulizoea kufanya shughuli hizi za uzinduzi makao makuu ya Mkoa na kuahidi kuwa ni mwanzo wa kufanya Shughuli za kimkoa na nyingine zitaendelea kufanyika Wilayani hapo.



"Kampeni hii itafanyika kwa siku 4 kuanzia tarehe 18 hadi 21 Mei 2022 ambapo lengo ni kuchanja watoto 846,733 katika Mkoa Mzima na kwa Wilaya ya Ukerewe inatakiwa kuchanja watoto 108,937." Amesema Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Dkt. Thomas Rutachunzibwa.

Dkt. Rutachunzibwa ameongeza kuwa Chanjo zitatolewa kupitia vituo 355 vikiwemo vituo 38 vya Wilaya ya Ukerewe na Watoa huduma 6,909 wamepata mafunzo kwa ajili ya kazi ya Uchanjaji, Watunza takwimu na wahamasishaji.



"Tumesambaza chanjo Dozi 973,740 katika vituo vyote na maandalizi ya kutoa chanjo hiyo yamekamilika na chanjo hii inatolewa bila malipo" Amesema Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Dkt. Thomas Rutachunzibwa.

Naye Diwani wa kata ya Nakatunguru, Mataba Sosthenes ameshukuru kwa uzinduzi wa kampeni ya Polio iliyofanyika katika kata yake na amemuomba Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe Mhandisi Robert Gabriel kuwasadia katika maboresho ya huduma mbalimbali katika kituo cha afya cha Nakatunguru.

Imetolewa na:
Kitengo cha Tehama
Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe.